# أسئلة مهمة

# Maswali muhimu

## *Yanayohusu maisha ya muislamu*

Mtunzi:

Shaykh, Faqiyh & Imaam Muhammad bin Swaalih bin ´Uthaymiyn

Tarjama:

Firqatunnajia.com

# Yaliyomo

01. Ni yepi maoni yako juu ya ambaye umebadilika ufahamu wake kiasi cha kwamba, mema yamekuwa maovu na maovu yamekuwa mema? .......... 4

02. Ni ipi hukumu ya kuwadhihaki wale wenye kushikamana na maamrisho ya Allaah na Mtume Wake? .......... 6

03. Ni ipi hukumu ya punyeto? .......... 8

04. Je, inafaa kwa mtu kutoka kwenda kuswali msikitini na akawaacha watoto wake nyumbani? .......... 9

05. Kipi afanye mtu akiwaamrisha familia yake kuswali lakini wasimuitikie? .......... 11

06. Ni ipi hukumu ya kukodisha maduka ya biashara kwa wale wanaouza sigara, nyimbo na kanda za video zisokuwa nzuri au benki za ribaa? .......... 15

07. Ni ipi hukumu ya kamari na yule anayedai kuwa inafaa? .......... 16

08. Je, inafaa kwa mwanamke kutoka kwenda sokoni pasi na kuwa na Mahram? Ni lini inafaa na lini inakuwa haramu? ... 17

09. Ni ipi hukumu ya kuvuta sigara na kuiuza? .......... 18

10. Ni ipi hukumu ya mchezo wa karata na sataranji? .......... 20

11. Ni ipi hukumu ya kunyoa ndevu au kuzikata na ni upi mpaka wake? .......... 21

12. Je, inafaa kuwatumia wafanyakazi wasiokuwa wa kiislamu? .......... 23

13. Ni ipi hukumu ya kusikiliza muziki na nyimbo pamoja na vipindi vya TV ambapo wanawake wanaonyesha mapambo yao? .......... 25

14. Ni ipi Hijaab inayokubalika kwa mujibu wa Shari´ah? .......... 27

15. Ni ipi hukumu ya kununua magazeti ya maonyesho ya mitindo kwa ajili ya kufunika nayo na mitindo mbalimbali ya mavazi ya wanawake? .......... 28

16. Ni ipi hukumu ya kukata nywele za wasichana kufika mabegani kwa ajili ya kujipamba, ni mamoja anyefanya hivo ameolewa au hakuolewa? .......... 29

17. Wasichana kuchelewesha kuolewa kwa sababu ya masomo na kazi ..................... 31

18. Ni ipi hukumu ya kufanya mazoezi kwa kaptula na ni ipi hukumu ya kuwatazama wanaofanya hivo? ..................... 32

19. Ni ipi hukumu ya kufanya kazi na kushirikiana na benki zenye ribaa? ..................... 33

20. Ni ipi hukumu ya mambo yanayofanywa na baadhi katika masherehe ya watu kupiga makofi na miluzi? ..................... 34

21. Je, ni haramu kuvaa nguo zinazovuka kongo mbili za miguu ikiwa ni pasi na kiburi au hapana? ..................... 35

**Kwa jina la Allaah, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu**

## 01. Ni yepi maoni yako juu ya ambaye umebadilika ufahamu wake kiasi cha kwamba, mema yamekuwa maovu na maovu yamekuwa mema?

**Swali 01:** Ni yepi maoni yako juu ya ambaye umebadilika ufahamu wake kiasi cha kwamba, mema yamekuwa maovu na maovu yamekuwa mema?

**Jibu:** Maoni yangu juu ya watu hawa ambao umebadilika ufahamu wao kiasi cha kwamba, wakaona mema ni maovu na maovu ni mema na hatimaye wakawa hawakemei chochote katika maovu na hawatambui chochote katika dini, naona kuwa wametoka nje ya dini – na tunamuomba Allaah ulinzi. Hivyo ni kwa sababu ambaye anaona mema, ambayo ni sehemu katika Shari´ah ya Allaah, kuwa ni maovu basi ameikufuru Shari´ah. Vivyo hivyo yule mwenye kuona maovu kuwa ni mema basi ameamini waungu wa batili na ukafiri. Imani haikamiliki isipokuwa kwa kukufuru waungu wa batili na ukafiri na sambamba na hilo mtu akamwamini Allaah. Ni lazima kwa watu hawa wazirejee nafsi zao, wafikirie hali zao, watambue msingi wao na mwisho wa jambo lao. Mwisho wao ni kutokuwepo na mwisho wa jambo lao ni kutokomea duniani. Amesema (Ta´ala):

هَلْ أَتَىٰ عَلَى الْإِنسَانِ حِينٌ مِّنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُن شَيْئًا مَّذْكُورًا

”Je, mtu hakufikiwa na kipindi fulani katika dahari, hakuwa kitu kinachotajwa?”[1]

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍوَيَبْقَىٰ وَجْهُ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

”Kila aliyekuwa humo [mbinguni na ardhini] atatoweka. Na utabakia uso wa Mola Wako wenye utukufu na wenye ukarimu.”[2]

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ وَإِنَّمَا تُوَفَّوْنَ أُجُورَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

”Kila nafsi itaonja mauti na hakika si vyenginevyo mtatimiziwa malipo yenu siku ya Qiyaamah.”[3]

[1] 76:01

[2] 55:26

Ni lazima kwao wayafikirie hayo kwa kina. Lisiposaidia, basi wafikirie tena kwa kina. Wanaona watu namna wanavyoondoka na kuja, wanazaana na wanakufa, wanagonjweka, wanapata uzima na wanapewa mtihani katika mali zao na familia zao. Wanajua kuwa hakuna yeyote atakayebaki katika duniani. Hivyo basi, warejee kwa Allaah (Ta´ala), watambue yaliyo mema na wayakemee yaliyo maovu. Hakika Allaah anamsamehe yule mwenye kutubia Kwake.

[3] 03:185

## 02. Ni ipi hukumu ya kuwadhihaki wale wenye kushikamana na maamrisho ya Allaah na Mtume Wake?

**Swali 02:** Ni ipi hukumu ya kuwachezea shere wale wenye kushikamana na maamrisho ya Allaah na Mtume Wake?

**Jibu:** Kuwafanyia istihzai wale wenye kushikamana na maamrisho ya Allaah na Mtume Wake kwa sababu wamelazimiana na mambo hayo, ni jambo la haramu na la khatari sana kwa mtu. Kwa sababu kunakhofiwa kule kuwachukia kwake ni kuichukia ile hali waliyomo ambayo ni kunyooka juu ya dini ya Allaah. Hivyo inakuwa maana yake, ni kuchezea shere ile njia waliyomo na hivyo wanakuwa wamefanana na wale ambao Allaah amesema juu yao:

قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ

“Sema: Je, mlikuwa mnamfanyia istihizai Allaah na Aayah Zake na Mtume Wake?” Msitoe udhuru; mmekwishakufuru baada ya kuamini kwenu.”[4]

Aayah hii imeteremka juu ya wanafiki waliosema:

”Hatujaona mfano wa wasomaji wetu hawa ambao wana matumbo makubwa, wanasema uwongo sana na ni waoga vitani.”

Wakimkusudia Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Maswahabah zake. Hapo ndipo Allaah akateremsha Aayah hii. Hivyo basi watahadhari wale wanaowafanyia dhihaka watu wa haki, kwa sababu wameshikamana na dini. Kwani Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) amesema:

إِنَّ الَّذِينَ أَجْرَمُوا كَانُوا مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا يَضْحَكُونَ وَإِذَا مَرُّوا بِهِمْ يَتَغَامَزُونَ وَإِذَا انقَلَبُوا إِلَىٰ أَهْلِهِمُ انقَلَبُوا فَكِهِينَ وَإِذَا رَأَوْهُمْ قَالُوا إِنَّ هَٰؤُلَاءِ لَضَالُّونَ وَمَا أُرْسِلُوا عَلَيْهِمْ حَافِظِينَ فَالْيَوْمَ الَّذِينَ آمَنُوا مِنَ الْكُفَّارِ يَضْحَكُونَ عَلَى الْأَرَائِكِ يَنظُرُونَ هَلْ ثُوِّبَ الْكُفَّارُ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ

“Hakika wale waliofanya ukhalifu walikuwa [duniani] wakiwacheka wale walioamini. Na wanapowapitia [karibu yao], basi wanakonyezana, na wanaporudi kwa familia zao, hurudi hali ya kuwa ni wenye kufurahika kwa kejeli, na wanapowaona, husema: “Hakika hawa bila shaka ndio waliopotea.” Hawakutumwa kuwa ni walinzi juu yao. Basi hii leo wale

[4] 09:65-66

walioamini watawacheka makafiri. Kwenye makochi ya fakhari wakitazama. Je, basi makafiri wamelipwa yale waliyokuwa wakiyafanya?"[5]

[5] 83:29-36

## 03. Ni ipi hukumu ya punyeto?

**Swali 03:** Ni ipi hukumu ya punyeto?

**Jibu:** Punyeto – ambako ni kule kujistarehesha kwa kutumia mkono au kitu kingine mfano wake – ni jambo la haramu kwa dalili ya Qur-aaan, Sunnah na utafiti sahihi. Kuhusu Qur-aan ni maneno Yake (Ta´ala):

وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ إِلَّا عَلَىٰ أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ فَمَنِ ابْتَغَىٰ وَرَاءَ ذَٰلِكَ فَأُولَـٰئِكَ هُمُ الْعَادُونَ

”Na wale ambao wanazihifadhi tupu zao, isipokuwa kwa wake zao au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, basi hao si wenye kulaumiwa. Basi yeyote yule atakayetaka kinyume ya hivo, basi hao ndio wavukao mipaka.”[6]

Yule ambaye anatafuta kukidhi matamanio yake kwa asiyekuwa mkewe au kijakazi wake, basi hakika ametaka kinyume na hivo na matokeo yake anakuwa amechupa mipaka kwa mujibu wa Aayah hii tukufu.

Kuhusu Sunnah, amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Enyi kongamano la barobaro! Yule atakayeweza miongoni mwenu kuoa basi na aoe. Hakika hilo linamfanya ainamishe macho na inahifadhi utupu wake. Yule asiyeweza basi ni juu yake afunge. Kwani kwake ni kinga.”[7]

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akamwamrisha ambaye hana uwezo wa kuoa afunge. Endapo kufanya punyeto ingekuwa ni jambo linafaa, basi angelielekeza Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Pale ambapo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakulielekeza – pamoja na wepesi wake – ndipo ikatambulika kuwa haijuzu.

Kuhusu utafiti sahihi, ni yale madhara makubwa yanayopelekea katika kitendo hichi. Madaktari wametaja kuwa linapelekea katika madhara makubwa yanayouathiri mwili, msukumo wa kujamiiana, fikira na tabia. Pengine hata likamzuilia kuoa, kwa sababu pengine mtu akapuuzilia mbali kuoa pale anapokidhi matamanio yake kwa njia kama hizi.

[6] 23:05-07

[7] al-Bukhaariy na Muslim.

## 04. Je, inafaa kwa mtu kutoka kwenda kuswali msikitini na akawaacha watoto wake nyumbani?

**Swali 04:** Je, inafaa kwa mtu kutoka kwenda kuswali msikitini na akawaacha watoto wake nyumbani?

**Jibu:** Ni lazima kwa mtu kutekeleza amri ya Allaah (´Azza wa Jall) pale aliposema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَائِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ لَّا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ

"Enyi mlioamini! Jikingeni nafsi zenu na familia zenu na Moto ambao mafutayake ni watu na mawe; juu yake wako Malaika wakali, shadidi hawamuasi Allaah kwa yale anayowaamrisha na wanafanya yale wanayoamrishwa."[8]

Ni lazima kwa mtu kuwaamrisha familia yake kuswali. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alifanya hivo pale aliposema:

"Waamrisheni watoto wenu kuswali wanapokuwa na miaka saba na wapigeni kwayo wanapokuwa na miaka kumi na watenganisheni kwenye malazi."[9]

Kadhalika Allaah (Ta´ala) ametaja kuwa Ismaa´iyl, ambaye ndiye baba wa waarabu:

وَكَانَ يَأْمُرُ أَهْلَهُ بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ وَكَانَ عِندَ رَبِّهِ مَرْضِيًّا

"Na alikuwa akiwaamrisha ahli zake swalah na zakaah na alikuwa mridhiwa mbele ya Mola wake."[10]

Haifai kwake kuwaacha watoto wake wanalala pasi na kuwaamsha kuswali na akawachunga. Haitoshi kuwaamsha peke yake, bali ni lazima kuwafuatilia. Pengine akawaamsha kisha wakarudi kulala. Ama kitendo cha yeye kutoka kwenda msikitini akawaacha nyumbani kwa sababu anachelea asipitwe na swalah ikiwa atabaki nyumbani na kuwachunga, anatakiwa kutoka kwenda kuswali kisha awarudilie. Hata hivyo akiwa ni mwenye kupuuza na anawaamsha pale anapotaka kutoka na hazumgumzi isipokuwa mara

[8] 66:06

[9] Ahmad na Abu Daawuud.

[10] 19:55

moja au mara mbili na anasema kuwa anachelea asije kupitwa na swalah, hakika kitendo hicho kinazingatiwa ni uzembe anaofanya. Bali analazimika kuwaamsha kutegemea na hali zao; kama wana uzito wa kuamka basi anapaswa kuwaamsha mapema na kinyume chake.

## 05. Kipi afanye mtu akiwaamrisha familia yake kuswali lakini wasimuitikie?

**Swali 05:** Kipi afanye mtu akiwaamrisha familia yake kuswali lakini wasimuitikie? Je, aishi pamoja nao na kuchanganyika nao au atoke ndani ya nyumba?

**Jibu:** Ikiwa wanafamilia hawa hawaswali kabisa, basi ni makafiri na wenye kuritadi. Wametoka nje ya Uislamu na haijuzu kuishi pamoja nao. Lakini ni lazima kwake kuwalingania, kuwang´ang´ania na akariri pengine Allaah akawaongoza. Kwa sababu mwenye kuacha swalah ni kafiri – na naomba ulinzi kwa Allaah. Hilo lina dalili ya Qur-aan, Sunnah, maneno ya Maswahabah na utafiti sahihi. Kuhusu ndani ya Qur-aan Tukufu Allaah (Ta´ala) amesema kuhusu washirikina:

فَإِن تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَإِخْوَانُكُمْ فِي الدِّينِ

"Wakitubu na wakasimamisha swalah na wakatoa zakaah, basi ni ndugu zenu katika dini."[11]

Kwa maana nyingine Aayah inasema wasipotekeleza swalah basi *sio* ndugu zenu. Udugu haukatiki kwa maasi, hata yakiwa makubwa kiasi gani, lakini udugu unakatika wakati mtu anapotoka katika Uislamu.

Kuhusiana na Sunnah Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Baina ya mtu na kufuru na shirki ni kuacha swalah."[12]

Amesema tena (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika Hadiyth ya Buraydah:

"Ahadi iliopo kati yetu sisi na wao ni swalah. Hivyo basi, yeyote atakayeiacha amekufuru."[13]

---

[11] 09:11

[12] at-Tirmidhiy ambaye amesema:

"Hadiyth hii ni nzuri na Swahiyh."

[13] an-Nawawiy amesema:

"Ameipokea at-Tirmidhiy katika "Kitaab-ul-Iymaan" kwa cheni ya wapokezi Swahiyh."

Ama maneno ya Maswahabah, amesema Kiongozi wa waumini ´Umar (Radhiya Allaahu ´anh):

"Hana fungu katika Uislamu kwa yule mwenye kuacha swalah."

Kwa sababu makanusho yamekuja kwa njia ya uhakika, basi ni yenye kuenea; si fungu kubwa wala dogo. ´Abdullaah bin Shaqiyq amesema:

"Hakuna kitu katika matendo Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) walikuwa wakiona kukiacha ni ukafiri isipokuwa swalah."

Kuhusu mtazamo sahihi kunasemwa: je, inaingia akilini kwa mtu ambaye moyoni mwake mna imani sawa na mbegu ya haradali, anajua utukufu wa swalah, namna Allaah alivyoitilia umuhimu, kisha asiichunge? Nimezingatia dalili za wale ambao hawaonelei mwenye kuacha swalah hakufuru, na nikaona kuwa hazitoki nje ya maoni manne:

1 – Hakuna dalili katika msingi wake.

2 – Zimefungamanishwa na sifa zinazokanusha kuacha swalah.

3 – Zimefungamanishwa na hali ya kumpa udhuru mwenye kuacha swalah.

4 – Zimekuja kwa njia ya kuenea na hivyo zikafanywa maalum na Hadiyth kuhusu ukafiri wa mwenye kuacha swalah.

Ikishabainika kuwa ambaye anaacha swalah ni kafiri, basi anafuatiwa na hukumu zifuatazo:

1 – Si sahihi kumuozesha. Akiozeshwa ilihali haswali, basi ndoa inazingatiwa ni batili na mwanamke huyo si halali kwake. Hilo ni kutokana na maneno Yake (Ta´ala) kuhusu wale wanawake waliohama:

لَا هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّونَ لَهُنَّ

"Wao [wanawake wa kiislamu] si halali kwao [hao makafiri] na wala wao [waume] si halali kwao."[14]

[14] 60:10

Akiacha swalah *baada* ya kuozeshwa, basi ndoa yake inafutika na mwanamke huyo si halali kwake. Dalili ya hilo ni Aayah ambayo tumeitaja punde.

2 – Mtu huyu ambaye haswali akichinja basi hakitoliwa kichinjwa chake. Kwa nini? Kwa sababu ni haramu. Hata hivyo endapo myahudi au mkristo atachinja basi vichinjwa vyao ni halali kwetu kuvila. Kwa hivyo kichinjwa chake kinakuwa kibaya zaidi kuliko kichinjwa cha myahudi na mkristo.

3 – Si halali kwake kuingia Makkah au mipaka yake mitakatifu. Amesema (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَٰذَا

”Enyi walioamini! Hakika washirikiana ni najisi, hivyo basi wasikaribie al-Masjid al-Haraam baada ya mwaka wao huu.”[15]

4 – Akifariki mmoja katika ndugu zake, basi hana haki ya kumrithi. Ni nani anayemrithi muislamu aliyekufa, hata hivyo anaye mtoto ambaye haswali na anaye binamu wa mbali anayeswali? Atamrithi huyo binamu yake wa mbali. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema katika Hadiyth ya Usaamah:

“Muislamu hamrithi kafiri wala kafiri hamrithi muislamu.”[16]

5 – Akifa, basi hatooshwa wala hatovikwa sanda. Aidha hatoswaliwa wala hatozikwa na waislamu. Tumfanye nini sasa? Tutatoka naye jangwani na kumchimbia shimo na kumzika akiwa na nguo yake, kwa sababu hana heshima yoyote. Kujengea juu ya hili haifai kwa mtu ambaye amefiwa na ndugu na yeye anatambua kuwa mtu huyo haswali, akamleta kwa waislamu wamswalie.

6 – Atafufuliwa siku ya Qiyaamah akiwa na Fir´awn, Haamaan, Qaaruun na Ubayy bin Khalaf[17] – na naomba ulinzi kwa Allaah. Aidha hatoingia Peponi na si halali kwa yeyote katika familia yake kumuombea du´aa ya rehema na msamaha, kwa sababu ni kafiri na hastahiki kuombewa hivo.

[15] 09:28

[16] al-Bukhaariy na Muslim.

[17] Ahmad (6288) na ad-Daarimiy (2605).

Enyi ndugu! Suala hili ni la khatari sana. Kwa masikitiko tunaona baadhi ya watu wanachukulia wepesi suala hili na wanawakubali wanafamilia wasioswali. Kitendo hichi hakijuzu na Allaah ndiye mjuzi zaidi.

Swalah na amani zimwendee Mtume wetu Muhammad, kizazi chake na Maswahabah zake.

## 06. Ni ipi hukumu ya kukodisha maduka ya biashara kwa wale wanaouza sigara, nyimbo na kanda za video zisokuwa nzuri au benki za ribaa?

**Swali 06:** Ni ipi hukumu ya kukodisha maduka ya biashara kwa wale wanaouza sigara, nyimbo na kanda za video zisokuwa nzuri au benki za ribaa?

**Jibu:** Hukumu ya kukodisha maduka haya inabainika katika maneno Yake (Ta´ala):

وَتَعَاوَنُوا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدْوَانِ

"Saidiane katika wema na kumcha Allaah na wala msisaidiane katika dhambi na uadui."[18]

Kutokana na hili kukodisha maduka kwa ajili ya utumiwaji uliyotajwa katika swali ni haramu. Kwa sababu ni kusaidiana katika dhambi na uadui.

[18] 05:02

## 07. Ni ipi hukumu ya kamari na yule anayedai kuwa inafaa?

**Swali 07:** Ni ipi hukumu ya kamari na yule anayedai kuwa inafaa?

**Jibu:** Kamari ni kitu kinatambulika kwa watu wengi na maana yake ni pale ambapo wanatofautiana watu wawili ambapo mmoja wao anasema: "Ikiwa mambo ni hivyo ulivosema, basi mimi nakupa hiki na hiki, na kama mambo ni vile ulivosema, basi nawe utanipa hiki na hiki." Jambo hilo halijuzu kwa sababu ni kamari, jambo ambalo Allaah (´Azza wa Jall) ameliambatanisha na pombe. Amesema (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنصَابُ وَالْأَزْلَامُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَن يُوقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَن ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنِ الصَّلَاةِ ۖ فَهَلْ أَنتُم مُّنتَهُونَ

"Enyi walioamini! Hakika si vyenginevyo pombe na kamari na kuabudu masanamu na kutazamia kwa mishale ya kupigia ramli ni uchafu kutokana na kazi ya shaytwaan, hivyo basi jiepusheni navyo mpate kufaulu. Hakika si venginevyo shaytwaan anachotaka kukutilieni kati yenu uadui na bughudha katika pombe na kamari na akuzuieni kumdhukuru Allaah na swalah, basi, je, mtakoma?"[19]

Kutokana na hilo kamari hii ni haramu. Kitendo cha baadhi ya watu kuona kuwa inafaa, haizidishi kitu isipokuwa ubaya tu. Kwa sababu ameifanya batili kuwa ni haki na ameipa jina lisilokuwa lake. Amelipamba na kuifanya ndio suluhisho. Kwa hivyo anakuwa ni mwongo katika yale aliyoyadai na mwenye kuhadaa katika yale anayoyadhihirisha – tunamuomba Allaah usalama na afya.

[19] 05:90-91

## 08. Je, inafaa kwa mwanamke kutoka kwenda sokoni pasi na kuwa na Mahram? Ni lini inafaa na lini inakuwa haramu?

**Swali 08:** Je, inafaa kwa mwanamke kutoka kwenda sokoni pasi na kuwa na Mahram? Ni lini inafaa na lini inakuwa haramu?

**Jibu:** Kimsingi ni kuwa inafaa kwa mwanamke kutoka kwenda sokoni. Si sharti awe na Mahram isipokuwa pale atapochelea fitina. Katika hali hiyo itamlazimu akitoka awe na Mahram wa kumlinda na kumuhifadhi. Ni sharti ili ifae kwake kutoka kwenda sokoni, atoke akiwa si mwenye kuonyesha mapambo na wala mwenye kujitia manukato. Akitoka hali ya kuwa ni mwenye kuonyesha mapambo au mwenye kujitia manukato, itakuwa si haramu kwake. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Msiwazuie wajakazi wa Allaah kutokamana na misikiti ya Allaah na watoke pasi na manukato wala kuonyesha mapambo."[20]

Jengine ni kwa sababu kutoka kwao hali ya kuonyesha mapambo au kujitia manukato, kunatokea fitina kupitia wao na kutoka kwao. Kukiaminika fitina na mwanamke akatoka kwa njia inayotakikana – pasi na kuonyesha mapambo wala kujitia manukato – basi kutakuwa hakuna ubaya kwake kutoka. Wanawake katika zama za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) walikuwa wakitoka kwenda katika masoko pasi na kuwa na Mahram.

[20] Ahmad na Abu Daawuud.

## 09. Ni ipi hukumu ya kuvuta sigara na kuiuza?

**Swali 09:** Ni ipi hukumu ya kuvuta sigara na kuiuza?

**Jibu:** Kuuza sigara ni haramu na vivyo hivyo inahusu kuinunua, kuiuza, kuwakodishia maduka wale wauzaji kwa sababu kufanya hivo maana yake ni kusaidiana katika dhambi na uadui. Dalili ya uharamu wake ni maneno Yake (Ta´ala):

وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ قِيَامًا

"Wala msiwape wasiokomaa kiakili mali yenu ambayo Allaah ameifanya kuwa ni kisaidizi chenu cha maisha."[21]

Dalili tumetumia ni kwa njia ya kwamba Allaah (Ta´ala) ametukataza kuwapa wapumbavu mali, kwa sababu mpumbavu atazitumia katika mambo yasiyokuwa na manufaa. Aidha amebainisha (Subhaanah) ya kuwa fedha hizi watu wanazitumia katika mambo yenye manufaa katika dini na dunia yao. Kwa maana nyingine kuzitumia katika sigara hakuna manufaa katika dini wala dunia. Kwa hivyo kuzitumia katika jambo hilo kunapingana na yale aliyowawekea Allaah (Ta´ala) Shari´ah waja Wake. Miongoni mwa dalili za uharamu wake ni maneno Yake (Ta´ala):

وَلَا تَقْتُلُوا أَنفُسَكُمْ

"Wala msiziue nafsi zenu."[22]

Kinacholengwa katika Aayah ni kuwa ni jambo limethibiti kidaktari ya kwamba uvutaji sigara unapelekea katika maradhi yasiyopona yanayompelekea mwenye nayo kwenye kifo kama vile kansa. Kwa hiyo mwenye kuitumia amefanya sababu ya kumwangamiza. Dalili nyingine ya uharamu wake ni maneno Yake (Ta´ala):

وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا ۚ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ

"Kuleni na kunyweni na wala msifanye israfu. Kwani Yeye hapendi wanaofanya israfu."[23]

[21] 04:05

[22] 04:29

[23] 07:31

Kinacholengwa katika Aayah hii ni kwamba ikiwa Allaah amekataza israfu katika mambo yanayofaa, basi makatazo ya kutumia pesa katika mambo yasiyokuwa na manufaa yatakuwa na nguvu zaidi.

Miongoni mwa dalili za uharamu wake ni kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekataza kuharibu pesa. Hapana shaka yoyote kwamba kutumia mali katika kununua sigara ni kuharibu pesa. Pesa ikitumiwa katika mambo yasiyokuwa na faida yoyote basi huko ni kuiharibu kusikokuwa na shaka. Zipo dalili nyinginezo. Akili inatosheka na dalili moja kutoka katika Kitabu cha Allaah au kutoka katika Sunnah zake Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam).

Kuhusu mtazamo sahihi unaofahamisha juu ya uharamu wake ni kwamba kila mwenye busara hawezi kutumia kitu ambacho kinampelekea kuumwa na kuuguwa. Kwa sababu ni lazima kwa mwenye akili kuhifadhi mwili na pesa zake. Hakuna anayepuuza hilo isipokuwa ambaye ni punguani katika akili na kufikiria kwake.

Dalili za kinadharia juu ya uharamu wake ni kwamba mvutaji akikosa sigara basi anahisi dhiki moyoni mwake, mkanganyiko na mawazo na moyo wake hauchamgamki isipokuwa akiipata. Miongoni mwa dalili za kinadharia juu ya uharamu wake ni kwamba mvutaji hupata ugumu wa kufanya ´ibaadah na khaswa swawm. Mvutaji hupata uzito mkubwa wa kufunga kwa sababu amezuiwa kuivuta kuanzia kuchomoza kwa alfajiri mpaka kuzama kwa jua. Katika kipindi cha majira ya joto ambapo mchana unakuwa mrefu pengine swawm inakuwa yenye kuchukiza kwake.

Mimi nawanasihi ndugu zangu waislamu wote kwa jumla na khaswa wale waliopewa mtihani watahadhari kutokana na jambo hilo. Ni mamoja kwa njia ya kununua, kuuza, uvutaji na kukodisha maduka kwa ajili ya kufanya biasara hiyo na kusaidia kwa njia yoyote ile.

## 10. Ni ipi hukumu ya mchezo wa karata na sataranji?

**Swali 10:** Ni ipi hukumu ya mchezo wa karata na sataranji?

**Jibu:** Wanazuoni (Rahimahumu Allaah) wamesema kuwa michezo hiyo ni haramu, kama walivoyataja hayo wanazuoni wetu. Hilo ni kutokana na ule upotofu mwingi unaopatikana katika jambo hilo na kuzuia kutokamana na utajo wa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Pengine vilevile likapelekea katika uadui na chuki kati ya wachezaji. Mara nyingi michezo hii inachezwa kwa zawadi, inatambulika ya kwamba kucheza kwa ajili ya zawadi ni jambo halijuzu isipokuwa katika yale mambo yaliyotajwa na Shari´ah, nayo ni mambo matatu: kulenga shabaha, khofu na kwato. Yule mwenye kuzingatia hali za wachezaji sataranji na karata, basi ataona kuwa wanapoteza wakati mrefu katika mambo yasiyokuwa ya kumtii Allaah na yasiyokuwa na faida. Baadhi ya watu wanasema kuwa kucheza karata na sataranji unafungua ubongo na kuikuza akili, lakini ukweli mambo ni kinyume na vile wanavyodai watu hawa. Bali ni jambo linadumaza akili na kuifanya akili ni yenye kufupika. Ikiwa mtu atazitumia fikira zake kwa njia nyingine, hatopata kitu, kwa sababu akili imedumazwa na kufupika katika jambo hili. Kwa ajili hiyo ni lazima kwa mwenye busara kujiepusha na michezo hiyo.

## 11. Ni ipi hukumu ya kunyoa ndevu au kuzikata na ni upi mpaka wake?

**Swali 11:** Ni ipi hukumu ya kunyoa ndevu au kuzikata na ni upi mpaka wake?

**Jibu:** Kunyoa ndevu ni haramu kwa sababu mtu anajifananisha na washirikina na waabudia moto. Mtume (Swalla Alaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Yeyote mwenye kujifananisha na watu basi yeye ni katika wao.”[24]

Aidha ni kubadilisha maumbile ya Allaah na kufuata maamrisho ya shaytwaan. Allaah (Subhaanah) amesema juu yake:

وَلَآمُرَنَّـهُمْ فَلَيُغَيِّرُنَّ خَلْقَ اللَّـهِ

"Nitawaamrisha watabadili uumbaji wa Allaah."[25]

Jengine ni kwamba mtu anaondosha yale maumbile ambayo Allaah amemuumba juu yake. Kuachia ndevu ni katika maumbile. Kadhalika ni kwenda kinyume na mwongozo wa waja wema wa Allaah ambao ni Manabii, Mitume na wale wafuasi wao. Ndevu zake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) zilikuwa nyeupe na nyingi na Allaah (Ta´ala) akaeleza kuwa Haaruun alimwambia ndugu yake Muusa (´alayhimaas-Salaam):

يَا ابْنَ أُمَّ لَا تَأْخُذْ بِلِحْيَتِي وَلَا بِرَأْسِي

“Ee mwana wa mama yangu! Usinishike ndevu zangu na wala kichwa changu.”[26]

Kwa hivyo kuzinyoa ni kutoka nje ya mwongozo wa waja wema wa Allaah ambao ni Manabii, Mitume na wengineo.

Kuzikata ni kuasi amri ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambaye alisema:

“Na ziacheni ndevu zikuwe.”[27]

---

[24] Ahmad na Abu Daawuud kwa cheni ya wapokezi ilio nzuri.

[25] 04:119

[26] 20:94

[27] al-Bukhaariy na wengineo.

“Fugeni ndevu.”

Inajulisha kuwa mwenye kupunguza kitu anakuwa amemuasi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), na ambaye amemuasi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) basi amemuasi vilevile Allaah. Allaah (Ta´ala) amesema:

مَّن يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ

“Atakayemtii Mtume, basi kwa hakika amemtii Allaah.”[28]

وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا

“Anayemuasi Allaah na Mtume Wake, basi hakika amepotoka upotofu wa wazi.”[29]

Utashangazwa na watu ambao wanasema kuwa kunyoa ndevu inafaa, licha ya kuwa wanajua kuwa ni katika desturi za waislamu, mwongozo wa Mitume na kujua kwao amri ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuziacha zikuwe. Licha ya hivo wanasema kuwa inafaa na kwenda kinyume na njia ya waumini.

Kwa mujibu wa maneno ya watu wa lugha mpaka wa ndevu ni nywele za kwenye kidevu na mashavuni. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

“Na ziacheni ndevu zikuwe.”

Neno “na” halikuziwekea ndevu mpaka kwa mujibu wa Shari´ah. Wakati yanapokuja maandiko pasi na mpaka uliowekwa katika Shari´ah, basi jambo hilo litachukuliwa kwa mujibu wa mpaka wa watu wa lugha, kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) anazungumza kwa lugha ya kiarabu na Qur-aan iko kwa kiarabu.

[28] 04:80

[29] 33:36

## 12. Je, inafaa kuwatumia wafanyakazi wasiokuwa wa kiislamu?

**Swali 12:** Je, inafaa kuwatumia wafanyakazi wasiokuwa wa kiislamu?

**Jibu:** Hapana shaka kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ameamrisha kuwatoa washirikina nje ya kisiwa cha kiarabu na akaamrisha kuwatoa mayahudi na manaswara nje ya kisiwa cha kiarabu. Amesema:

"Nitawatoa mayahudi na manaswara nje ya kisiwa cha kiarabu mpaka nisimwache isipokuwa muislamu peke yake."[30]

Hadiyth hii inajulisha kuwa mwongozo wa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ni kwamba kisiwa cha kiarabu kusibaki isipokuwa aliye muislamu peke yake. Hilo ni kutokana na ile khatari inayopatikana kwa uwepo wa manaswara na makafiri wengine katika kisiwa cha kiarabu. Uislamu umeanza kutokea katika kisiwa hichi cha waarabu na ukaenea katika kona zote za ulimwengu. Imethibiti kwa mapokezi Swahiyh ya kwamba imani itarudi Madiynah kama ambavyo nyoka anarudi ndani ya shimo lake. Mambo yakishakuwa hivo basi itambulike kuwa kuwatumia wasiokuwa waislamu ndani ya bara hili ni jambo lina khatari kubwa, ijapokuwa hakuna khatari na madhara mengine zaidi ya kule kutangamana nao, kuwategemea na pengine hata ikatokea kumpenda. Allaah (Ta´ala) amesema:

لَّا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّـهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّـهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ ۚ أُولَـٰئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ

"Hutopata watu wanaomuamini Allaah na siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wale wanaopinzana na Allaah na Mtume Wake, japo wakiwa ni baba zao, watoto wao, ndugu zao au jamaa zao. Hao [Allaah] amewaandikia katika nyoyo zao imani na akawatia nguvu kwa Roho kutoka Kwake."[31]

Huenda akafikia kutoona tofauti ya haki na batili na hatimaye akawaona kuwa ni ndugu zetu. Pengine shaytwaan akamfanya kuwaona kuwa ni ndugu zetu katika ubinaadamu,

[30] Muslim.

[31] 58:22

jambo ambalo si sahihi. Udugu wa kikweli ni ule udugu wa kiimani. Hakuna udugu kwa kutofautiana kwa dini. Wakati Nuuh aliposema:

رَبِّ إِنَّ ابْنِي مِنْ أَهْلِي وَإِنَّ وَعْدَكَ الْحَقُّ وَأَنتَ أَحْكَمُ الْحَاكِمِينَ

”Ee Mola wangu! Hakika mtoto wangu ni katika ahli zangu na hakika ahadi Yako ni ya kweli Nawe ni muadilifu zaidi wa kuhukumu kuliko mahakimu wote."[32]

Allaah akasema kumwambia:

يَا نُوحُ إِنَّهُ لَيْسَ مِنْ أَهْلِكَ

”Ee Nuuh! Hakika huyo si katika mwa ahli zako.”[33]

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amekata mahusiano kati ya waumini na makafiri mpaka katika kurithiana baada ya kufa. Amesema:

“Muislamu hamrithi kafiri wala kafiri hamrithi muislamu.”

Mambo yakishakuwa hivo, itambulike kuwa kuchanganyika na wasiokuwa waislamu, kuwatumia na kushirikiana nao makazini, kula, kunywa na matembezi yote haya yanapelekea kufisha ile ghera ndani ya mioyo ya waislamu mpaka anaingia ndani ya wale ambao Allaah (Ta´ala) amesema juu yao:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا عَدُوِّي وَعَدُوَّكُمْ أَوْلِيَاءَ تُلْقُونَ إِلَيْهِم بِالْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُوا بِمَا جَاءَكُم مِّنَ الْحَقِّ

“Enyi mlioamini! Msimchukue adui Wangu na adui wenu kuwa marafiki mkiwapelekea mapenzi na hali wamekwishakanusha haki iliyokujieni.”[34]

[32] 11:45

[33] 11:46

[34] 60:01

## 13. Ni ipi hukumu ya kusikiliza muziki na nyimbo pamoja na vipindi vya TV ambapo wanawake wanaonyesha mapambo yao?

**Swali 13:** Ni ipi hukumu ya kusikiliza muziki na nyimbo pamoja na vipindi vya TV ambapo wanawake wanaonyesha mapambo yao?

**Jibu:** Kusikiliza muziki na nyimbo ni haramu na hapana shaka juu ya uharamu wake. Imepokelewa kutoka kwa Salaf, ambao ni Maswahabah na wanafunzi wao, ya kwamba muziki unazalisha unafiki ndani ya moyo, maneno ya kipuuzi na unapelekea mtu kuegemea juu yake. Allaah (Ta´ala) amesema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَشْتَرِي لَهْوَ الْحَدِيثِ لِيُضِلَّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَيَتَّخِذَهَا هُزُوًا ۚ أُولَـٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مُّهِينٌ

“Miongoni mwa watu wako ambao hununua maneno ya upuuzi ili wapoteze kutokamana na njia ya Allaah pasi na elimu na huichukulia mzaha – hao watapata adhabu ya kutweza.”[35]

Ibn Mas´uud amesema wakati alipokuwa anafasiri Aayah hii:

“Naapa kwa Allaah ambaye hakuna mungu wa haki mwingine isipokuwa Yeye; ya kwamba ni nyimbo.”[36]

Tafsiri ya Swahabah ni hoja na iko katika ngazi ya tatu katika tafsiri, kwa sababu tafsiri ina ngazi tatu:

1 – Tafsiri ya Qur-aan kwa Qur-aaan.

2 - Tafsiri ya Qur-aan kwa Sunnah.

3 - Tafsiri ya Qur-aan kwa maneno ya Maswahabah.

Wapo mpaka baadhi ya wanazuoni wenye kuona kuwa tafsiri ya Swahabah ina hukumu moja kama ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Lakini maoni ya sawa ni kwamba haina hukumu moja. Lakini hata hivyo ndio maneno yaliyo karibu zaidi na haki.

---

[35] 31:06

[36] al-Bukhaariy na wengineo.

Isitoshe ni kwamba kusikiliza nyimbo na muziki ni kutumbukia katika yale ambayo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ametahadharisha pale aliposema:

"Hakika watakuweko katika Ummah wangu watu wataohalalisha uzinzi, hariri, pombe na zana za muziki."

Bi maana wataona kuwa uzinzi, pombe na hariri ni halali. Ni wanaume ambao haifai kwao kuvaa hariri. Zana za muziki ni ala za upuuzi. Ameipokea al-Bukhaariy kutoka kwa Abu Maalik al-Ash´ariy au Abu ´Amr al-Ash´ariy. Kutokana na hilo mimi nawatahadharisha ndugu zangu waislamu kusikiliza nyimbo na muziki na wala wasidanganyike na maoni ya baadhi ya wanazuoni waliosema kuwa zana za muziki zinafaa. Kwa sababu dalili zinazoharamisha ziko wazi kabisa.

Kuhusu kuangalia vipindi vya TV ambavyo wanaonekana wanawake ni haramu muda wa kuwa zinapelekea katika fitina na kuwa na mafungamano na wanawake. Mara nyingi vipindi vyote vya TV ni vyenye madhara hata kama mwanamme hamuoni mwanamke na mwanamke hamuoni mwanaume. Kwa sababu malengo yake huwa ni kuidhuru jamii katika maadili na tabia yake. Namuomba Allaah (Ta´ala) awakinge waislamu kutokana na shari yake na awatengeneze watawala wa waislamu katika yale yanayozitengeneza hali za waislamu na Allaah ndiye anajua zaidi.

## 14. Ni ipi Hijaab inayokubalika kwa mujibu wa Shari´ah?

**Swali 14:** Ni ipi Hijaab inayokubalika kwa mujibu wa Shari´ah?

**Jibu:** Hijaab inayokubalika kwa mujibu wa Shari´ah ni mwanamke kufunika yale anayoharamika kuyaonyesha. Kinachoshika nafasi ya kwanza ni kufunika uso, kwa sababu ndio sababu inayopelekea katika fitina na matamanio. Kwa hivyo ni lazima kwa mwanamke kuufunika uso wake mbele ya wasiokuwa Mahram zake. Kuhusu wale waliodai kuwa Hijaab inayokubalika kwa mujibu wa Shari´ah ni kufunika tu shingo, mgongo, miguu, miundi na mikono na akamruhusu mwanamke kuonyesha uso na viganja vyake vya mikono, ni miongoni mwa maoni yanayostaajabisha mno. Ni jambo linalotambulika kuwa matamanio na mahali palipo na fitina ni usoni. Ni vipi mtu anaweza kusema kuwa Shari´ah inamkataza mwanamke kuonyesha miguu halafu imruhusu kuonyesha uso? Hili ni jambo lisilowezekana katika Shari´ah tukufu na yenye hekima iliyotakasika kutokamana na mgongano.

Kila mtu anatambua kuwa fitina inayopatikana kwa kuonyesha uso ni kubwa zaidi kuliko fitina inayopatikana kwa kunyesha miguu. Kila mtu anajua kuwa matamamio ya wanamme juu ya wanawake yako usoni. Kwa ajili hiyo endapo ataambiwa yule mposaji kuwa mwanamke anayetaka kumposa sura yake ni mbaya, lakini hata hivyo miguu yake ni mizuri, basi hatomposa. Na endapo ataambiwa kuwa sura yake ni nzuri, lakini pamoja na hivyo mikono yake, viganja vyake vya mikono, miguu yake, miundi yake si mizuri sana, atamposa. Kwa ajili hiyo inapata kufahamika kuwa uso ndio kitu cha kwanza kinachotakiwa kufunikwa. Aidha zipo dalili ndani ya Kitabu cha Allaah, Sunnah za Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), maneno ya Maswahabah pamoja maneno ya maimamu na wanazuoni wa Uislamu zinazojulisha ulazima wa mwanamke kuufunika mwili wake mzima mbele ya wale wasiokuwa Mahram zake. Vilevile dalili hizo zinafahamisha kuwa ni lazima kwa mwanamke kuufunika uso wake mbele ya wasiokuwa Mahram zake, jambo ambalo hapa si mahali pake pa kulitaja na Allaah ndiye anajua zaidi.

## 15. Ni ipi hukumu ya kununua magazeti ya maonyesho ya mitindo kwa ajili ya kufunika nayo na mitindo mbalimbali ya mavazi ya wanawake?

**Swali 15:** Ni ipi hukumu ya kununua magazeti ya maonyesho ya mitindo kwa ajili ya kufunika nayo na mitindo mbalimbali ya mavazi ya wanawake? Ni ipi hukumu ya kubaki nayo baada ya kunufaika nayo na yamejaza picha za wanawake?

**Jibu:** Hapana shaka kuwa kununua magazeti ambayo hayana jengine zaidi ya picha ni haramu. Kwa sababu kuhifadhi picha ni haramu kutokana na maneno yake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Malaika hawaingii kwenye nyumba ilio ndani na picha."[37]

Jengine ni kuwa wakati alipoona picha kwenye mto wa ´Aaishah, alisimama na hakuingia ndani na akaona machukizo yake usoni mwake. Magazeti haya ambayo yanaonyesha fasheni yanatakiwa kukaguliwa na si kila nguo inafaa. Pengine nguo hizi zinazonyesha sehemu za siri za mtu ima kutokana na kubana kwake au mfano wake. Pengine vilevile mavazi haya ni miongoni mwa mavazi maalum ya makafiri, na kujifananisha na makafiri ni jambo la haramu. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Yeyote mwenye kujifananisha na watu basi yeye ni katika wao."[38]

Kwa hivyo kile ninachowanasihi ndugu zangu wote wa kiislamu na khaswa wanawake wa kiislamu wajiepushe na nguo hizi kwa sababu baadhi ya nguo zinakuwa na kujifananisha na wasiokuwa waislamu na nyenginezo zinaonyesha uchi. Jengine ni kwamba wanawake kutaka kuwa na kila vazi jipya linalotoka, mara nyingi litapelekea kubadilisha desturi zetu, ambazo chimbuko lake ni dini yetu, na kwenda katika desturi nyenginezo zenye kutoka kwa wasiokuwa waislamu.

[37] al-Bukhaariy, Muslim na wengineo.

[38] Ahmad na Abu Daawuud kwa cheni ya wapokezi ilio nzuri.

## 16. Ni ipi hukumu ya kukata nywele za wasichana kufika mabegani kwa ajili ya kujipamba, ni mamoja anyefanya hivo ameolewa au hakuolewa?

**Swali 16:** Ni ipi hukumu ya kukata nywele za wasichana kufika mabegani kwa ajili ya kujipamba, ni mamoja anyefanya hivo ameolewa au hakuolewa? Ni ipi hukumu ya kuvaa viatu vyenye visigino virefu, ni mamoja virefu sana au kidogo? Ni ipi hukumu ya kutumia zana za vipodozi vinavyotambulika kwa ajili ya kumpambia mume?

**Jibu:** Ni haramu kwa mwanamke kukata nywele zake kwa njia ya kufanana na nywele za wanamme na inahesabika ni miongoni mwa madhambi makubwa. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amewalaani wanawake wenye kujifananisha na wanamme. Hali nyingine ni kukata nywele kwa njia isiyokuwa na kufanana na wanamme, wanazuoni wametofautiana katika maoni matatu:

1 – Wako waliosema kuwa inafaa na hapana vibaya.

2 – Wengine wakasema kuwa ni haramu.

3 – Baadhi ya wengine wakasema kuwa inachukiza.

Kinachotambulika katika madhehebu ya Imaam Ahmad ni kwamba inachukiza. Ukweli wa mambo – kama tulivyotangulia kutaja katika jibu lililotangulia – ni kwamba haitakiwi kwetu kupokea kila desturi zisizokuwa zetu. Sisi muda si mrefu sana tulikuwa tunawaona wanawake wanajisifu ni nani kati yao mwenye nywele nyingi zaidi kichwani au mwenye nywele refu zaidi. Ni kwa nini basi wanayaendea matendo yaliyotoka nje ya nchi isiyokuwa yetu? Mimi sipingi kila kipya, lakini mimi napinga kila kitu ambacho kinapelekea jamii kwenda katika ada zinazotoka kwa wasiokuwa waislamu.

Kuhusu viatu vyenye kisigino kirefu havijuzu vinavyopingana na desturi na pia kupelekea kuonyesha mapambo na kuwafanya wanamme kumwelekezea macho. Allaah amesema:

وَقَرْنَ فِي بُيُوتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْأُولَى

"Tulizaneni majumbani mwenu na wala msijishauwe kwa kuonyesha mapambo kama walivyojishauwa zama za ujahili."[39]

[39] 33:33

Kila kitu ambacho maana yake ni kuonyesha mapambo na kudhihiri kwake na akajitofautisha na wanawake wengine kwa njia ya kujipamba, ni haramu na hakijuzu.

Kuhusu kutumia zana za vipodozi, kama kuifanya midomo kuwa miekundu na kuyafanya mashavu kuwa mekundu, haina neno na khaswa ikiwa ni mwanamke aliyeolewa. Kuhusu mapambo yanayofanywa na baadhi ya wanawake ambapo wanaondosha na kuchonga nyusi ni haramu. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amewalaani wanawake wenye kuchonga na wenye kuchongwa nyusi na pia mwanamke mwenye kuyapamba meno yake ili yaonekane mazuri.

## 17. Wasichana kuchelewesha kuolewa kwa sababu ya masomo na kazi

**Swali 17:** Kuna ada iliyoenea ambayo ni msichana kukataa kuolewa au baba yake kumkatalia yule mposaji ili akamilishe masomo yake ya sekondari, chuo kikuu au masomo kwa muda wa miaka kadhaa. Ni ipi hukumu ya hilo na ni zipi nasaha zako kwa wenye kufanya hivo? Wakati mwingine wanawake wanaenda mpaka miaka thelathini au zaidi na bado hawajaolewa.

**Jibu:** Hukumu ya hilo ni kwenda kinyume na amri ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Atapokujieni yule ambaye mmeiridhia dini na tabia yake basi muozesheni."

"Enyi kongamano la vijana! Yule miongoni mwenu mwenye uwezo wa kuoa na afanye hivyo, kwani hilo linamfanya ainamishe macho yake na inahifadhi utupu wake."

Kujizuilia na ndoa kunapelekea kukosa manufaa mengi ya ndoa. Kwa ajili hiyo nawanasihi ndugu zangu waislamu ambao ndio wasimamizi wa wanawake na pia dada zangu wa kiislamu, wasikatae kuolewa kwa sababu ya kukamilisha masomo. Wanachoweza kufanya ni mwanamke kumuwekea sharti mwanamme kuendelea na masomo yake mpaka atakapomaliza, au kuendelea na kazi yake ya kufundisha kwa kipindi cha mwaka mmoja au miaka miwili, muda wa kuwa hakushughulishwa kutokamana na watoto wake. Mwanamke kuzama katika elimu ya vyuo vikuu, ambazo hatuzihitaji, ni jambo linatakiwa kuangaliwa vyema. Kile ninachoona ni kuwa inatosha kwa mwanamke kumaliza masomo yake ya hatua ya awali na akawa anajua kusoma na kuandika kwa njia ya kwamba atanufaika kwa elimu yake hii kuweza kusoma Kitabu cha Allaah, tafsiri yake na kusoma Hadiyth za Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na maelezo yake. Labda azame kusoma elimu ambazo watu wanazihitaji kama mfano wa elimu ya udaktari na mfano wake muda wa kuwa katika kusoma kwake hakuna mambo yanayokataliwa na Shari´ah kama vile kuchanganyika kwa wanamme na wanawake na mambo mfano wake.

## 18. Ni ipi hukumu ya kufanya mazoezi kwa kaptula na ni ipi hukumu ya kuwatazama wanaofanya hivo?

**Swali 18:** Ni ipi hukumu ya kufanya mazoezi kwa kaptula na ni ipi hukumu ya kuwatazama wanaofanya hivo?

**Jibu:** Kufanya mazoezi ni jambo linafaa ikiwa hayamshugulishi mtu na jambo la wajibu. Vinginevyo itakuwa haramu. Ikiwa mtu hana kazi nyingine isipokuwa hii kwa njia ya kwamba yanamchukua muda wake mwingi, inazingatiwa ni kupoteza wakati na dogo liwezalo kusemwa katika hali hii ni kuwa inachukiza.

Lakini ikiwa wafanyaji mazoezi wamevaa kaptula kwa njia ya kwamba paja, sehemu yake kubwa inaonekana, basi haitojuzu. Maoni sahihi ni kwamba ni lazima kufunika mapaja na haijuzu kuwatazama wachezaji wakiwa katika hali kama hii.

## 19. Ni ipi hukumu ya kufanya kazi na kushirikiana na benki zenye ribaa?

**Swali 19:** Ni ipi hukumu ya kufanya kazi na kushirikiana na benki zenye ribaa?

**Jibu:** Kufanya kazi ni haramu. Kwa sababu maana yake ima ni kusaidiana juu ya ribaa – jambo ambalo linaingia ndani ya laana ya mlaanaji Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ambapo imesihi kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba amemlaani mwenye kula ribaa, mwenye kuitoa, katibu wake na mwenye kuishuhudia na akasema kuwa wote wana hukumu moja – au ni kuridhia na kukubaliana na kitendo hichi. Haijuzu kuajiriwa katika mabenki yanayofanya kazi na ribaa. Hata hivyo hapana vibaya kuhifadhi pesa kutokana na haja ikiwa hatukupata njia nyingine ya kuzihifadhi. Katika hali hii hapana vibaya, kwa sharti mtu asichukue ribaa kutoka humo. Hata hivyo itakuwa haramu endapo mtu atachukua ribaa.

## 20. Ni ipi hukumu ya mambo yanayofanywa na baadhi katika masherehe ya watu kupiga makofi na miluzi?

**Swali 20:** Ni ipi hukumu ya mambo yanayofanywa na baadhi katika masherehe ya watu kupiga makofi na miluzi?

**Jibu:** Hukumu ya hayo ni kwamba yametoka kwa wasiokuwa waislamu. Kwa ajili hiyo haitakiwi kwa waislamu kuyafanya. Badala yake anatakiwa kusema "Allaahu Akbar" au "Subhaan Allaah" pindi jambo linapomfurahisha. Hata hivyo haya hayatakiwi kufanywa kwa pamoja, kama wanavofanya baadhi ya watu, bali mmojammoja. Kuhusu kusema "Allaahu Akbar" au "Subhaan Allaah" kwa njia ya pamoja wakati kunapotea kitu cha kufurahisha, ni jambo halina msingi wowote kutokana na ninavyojua.

## 21. Je, ni haramu kuvaa nguo zinazovuka kongo mbili za miguu ikiwa ni pasi na kiburi au hapana?

**Swali 21:** Je, ni haramu kuvaa nguo zinazovuka kongo mbili za miguu ikiwa ni pasi na kiburi au hapana?

**Jibu:** Wanamme kuvaa nguo inayovuka tindi mbili za miguu ni haramu. Ni mamoja mtu amefanya hivo kwa kiburi au bila kiburi. Lakini ikiwa kumeambatana na kiburi basi adhabu yake ni kubwa na mbaya zaidi kutokana na Hadiyth ya Abu Dharr iliyothibiti katika "as-Swahiyh" ya Muslim ambaye amesimulia ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Watu aina tatu hatowasemeza Allaah siku ya Qiyaamah, hatowatakasa na watakuwa na adhabu kali." Abu Dharr akasema: "Ni kina nani, ee Mtume wa Allaah, wamekula patupu na wamekhasirika?" Akasema: "Mwanaume mwenye kuvaa nguo ndefu yenye kuvuka kongo mbili za miguu, mzee mzinifu, mtu fakiri mwenye kiburi na mtu ambaye kamfanya Allaah ndio bidhaa yake; hanunui isipokuwa kwa kuapa na wala hauzi isipokuwa kwa kuapa."[40]

Hadiyth hii ni yenye kuenea, lakini hata hivyo inafanywa maalum kwa Hadiyth ya Ibn ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa) ambapo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Allaah hatomtazama ambaye anaburuza nguo yake kwa kiburi."[41]

Kwa hivyo ueneaji katika Hadiyth ya Abu Dharr unafanywa maalum kwa Hadiyth ya Ibn ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa). Ikishakuwa anafanya hivo kwa kiburi basi Allaah hatomtazama, hatomtakasa na pia atakuwa na dhabu kali. Adhabu hii ni kubwa zaidi kuliko adhabu atayopata yule ambaye anaburuza nguo yake chini ya kongo mbili za miguu pasi na kiburi. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema juu ya mtu huyo:

"Kile kilicho chini ya kongo mbili za miguu katika kikoi ni Motoni."[42]

---

[40] Muslim, Abu Daawuud, an-Nasaa´iy na Ibn Maajah.

[41] al-Bukhaariy.

[42] al-Bukhaariy na Ahmad.

Pindi ilipokuwa adhabu mbili zinatofautiana, basi kunazuilika maandiko yaliyoachiwa kuyafasiri yaliyofungwa. Kwa sababu ili maandiko yaliyoachiwa kuyafasiri yaliyofungwa ni sharti maandiko hayo mawili yawe na hukumu moja. Lakini ikiwa hukumu inatofautiana, basi andiko moja haliwezi kufungamanishwa na jengine. Kwa ajili hiyo Aayah inayozungumzia Tayammum ambapo Allaah (Ta´ala) amesema:

وَإِن كُنتُمْ جُنُبًا فَاطَّهَّرُوا ۚ وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ الْغَائِطِ أَوْ لَامَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُم مِّنْهُ

“Mkiwa na janaba, basi jitwaharisheni na mkiwa wagonjwa au mko safarini au mmoja wenu akija kutoka msalani au mmewagusa wanawake kisha hamkupata maji, basi fanyeni Tayammum kwa ardhi kwa juu panguseni kwayo nyuso zenu na mikono yenu.”[43]

hatukuifungamanisha na Aayah ya wudhuu´ inayosema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ

“Enyi mlioamini! Mnaposimama kwa ajili ya swalah, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka kwenye visugudi.”[44]

Kwa ajili hiyo Tayammum haitambai kwenda mpaka kwenye visugudi. Kinachofahamisha hayo ni yale aliyopokea Maalik na wengineo kutoka katika Hadiyth ya Abu Sa´iyd al-Khudriy ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisema kuwa kikoi cha muumini ni mpaka kwenye nusu ya muundi wake, kwamba kile kilicho chini ya kongo mbili za miguu katika kikoi ni Motoni na kwamba Allaah hatomtazama ambaye anaburuza nguo yake kwa kiburi. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akataja mifano miwili katika Hadiyth moja na akabainisha kutofautiana kwa hukumu zake kwa kutofautiana kwa adhabu zao. Ni wenye kutofautiana katika kitendo na pia ni wenye kutofautiana katika hukumu na adhabu. Kutokana na haya yanabainika makosa ya wale ambao wamefungamanisha maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

“Kile kilicho chini ya kongo mbili za miguu katika kikoi ni Motoni.”

kwa maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

[43] 05:06

[44] 05:06

“Allaah hatomtazama ambaye anaburuza nguo yake kwa kiburi.”

Licha ya haya wapo watu pindi wanapokatazwa kuvaa nguo inayovuka kongo mbili za miguu wanasema kuwa wao hawavai kwa kiburi. Tunawaambia kuna sampuli mbili za nguo inayovuka kongo mbili za miguu. Aina ya kwanza ya adhabu ni mtu kuadhibiwa yale maeneo aliyotenda dhambi peke yake, nacho ni kile kilicho chini ya mafundo mawili ya miguu pasi na kiburi. Huyu ataadhibiwa na Allaah ikiwa ni pamoja na kutomtazama na kutomtakasa. Lakini yule anayeburuza nguo zake kwa kiburi Allaah atamuadhibu kwa kutomsemeza, hatomtazama wala hatomtakasa siku ya Qiyaamah na atakuwa na adhabu kali. Hivi ndivo tunavyomwambia.

Swalah na amani zimwendee Mtume wetu Muhammad, kizazi chake na Maswahabah zake.